# TAARIFA KWA UMMA

**TANGAZO HILI LIMEIDHINISHWA NA MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA (CMSA)**

**UTOAJI WA HISA ZA UPENDELEO 72,957,660 ZA KAMPUNI YA UWEKEZAJI TCCIA (TCCIA INVESTMENT PLC)**

TCCIA Investment PLC inatoa taarifa kwa umma kuwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, imeidhinisha Waraka wa Matarajio wa TCCIA Investment Plc kuuza hisa za upendeleo 72,957,660 kwa wanahisa wake kwa bei ya Shilingi 145 kwa kila hisa.

**TAARIFA YA UTOAJI WA HISA ZA UPENDELEO ZA TCCIA INVESTMENT PLC:**

Muhtasari wa taarifa muhimu kuhusu hisa za upendeleo za TCCIA Investment Plc zimewekwa hapa chini:

| | |
|---|---|
| Mtoaji: | TCCIA Investment PLC |
| Bei: | Shilingi 145 Kwa kila hisa |
| Idadi ya hisa zinazotolewa: | Hisa 72,957,660 |
| Mtaji uliokusudiwa kukusanywa: | Shilingi 10,578,860,700 |
| Uwiano wa hisa za upendeleo: | Hisa 1 mpya kwa kila hisa 1 iliyopo |

Uwekezaji unafanyika kwa njia Wanahisa kujaza fomu za maombi zitakazotumwa kwao. Wanahisa wanashauriwa kusoma waraka wa matarajio na fomu za maombi zitakazotumwa. Waraka wa matarajio unapatikana kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya TCCIA Investment PLC www.tcciainvestment.com na kupitia Mshauri Kiongozi (iTrust Finance Limited): Barua pepe: tcciarightsissue@itrust.co.tz

Maombi yatakamilishwa kwa kufanya malipo katika akaunti ya CRDB Bank PLC iliyoorodheshwa hapo chini:

**Akaunti ya Malipo**

| | |
|---|---|
| TCCIA RIGHTS ISSUE COLLECTION ACCOUNT | **01DI011240700** |

**TAREHE ZA MATUKIO MUHIMU**

| | Tukio | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. | Tarehe ya mwisho kununua Hisa | **Jumatatu, 06 November 2023** |
| 2. | Tarehe ya Rekodi | **Alhamis, 09 November 2023** |
| 3. | Usambazaji wa Fomu kwa wanahisa | **Ijumaa, 10 November 2023** |
| 4. | Kufungua Mauzo ya Hisa za Upendeleo | **Ijumaa, 10 November 2023** |
| 5. | Kufunga Mauzo ya Hisa za Upendeleo | **Ijumaa, 01 December 2023** |
| 6. | Tangazo la matokeo ya Mauzo ya Hisa | **Ijumaa, 08 December 2023** |
| 7. | Kuorodheshwa kwa Hisa DSE | **Alhamis, 14 December 2023** |

Wawekezaji wanashauriwa kuwasiliana na mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam wenye leseni kutoka Mamlaka ya Masoko, Mitaji na Dhamana (CMSA); wahasibu, wanasheria au washauri wengine wa masuala ya fedha kwa ushauri elekezi ili kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji.

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mtendaji,**
**TCCIA Investment PLC**
**Millenium Tower II,**
**Ghorofa ya 24, S.L.P 72678,**
**Dar es Salaam, Tanzania.**